Kwa mfano, kiwango cha uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka wastani wa gunia 5 hadi 20 kwa ekari.

### 4.3 Uzingatiwaji wa mahitaji halisi ya wakulima:

Matokeo ya utafiti unaonyesha kuwa utoaji wa pembejeo za kilimo haukuzingatia mahitaji halisi ya wakulima. Katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji wa mazao ya mahindi mbolea iliyopelekwa hasa Minjingu imeonekana kutokuwa sahihi na mahitaji halisi ya udongo wa maeneo husika. Na katika maeneo ya wakulima wa mazao ya biashara hasa pamba, madawa yaliyopelekwa hayakuwa na sifa wakulima wanazozihitaji. Kwa mfano wakulima wa pamba hitaji lao ni madawa aina ya mafuta badala ya maji.

## 5.0 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Ili kuhakikisha lengo la kumwezesha mkulima mdogo kumudu gharama za matumizi ya pembejeo linafikiwa, utafiti unapendekeza yafuatayo:

- Utoaji wa pembejeo upitie vikundi badala ya mkulima mmoja mmoja. Katika vikundi wakulima wanajuana na sio rahisi pembejeo kupelekwa nje ya walengwa.
- Kuwe na warsha za mafunzo kwa walengwa na wadau mbalimbali juu ya muundo na utekelezaji wa mfumo huu.

Timu huru za ufuatiliaji zinazowakilisha wadau mbalimbali ziundwe katika ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji ili kubaini na kuboresha upatikanaji wa pembejeo hizo kwa walengwa.

Utoaji wa pembejeo ufanyike kutokana na mahitaji ya mkulima na hali halisi ya virutubisho (kama vile N, P, K) vilivyopungua kwenye udongo.

Serikali ije na utaratibu wa upimaji wa udongo wenye gharama nafuu (simple soil testing kit) ili wakulima wadogo wadogo waweze kumudu gharama za uchambuzi wa udongo na hivyo kutambua mahitaji halisi ya uboreshaji wa udongo.



Uchakachuaji wa pembejeo


Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

*Uongozi wa Mradi wa EPINAV*

*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo*

*S. L. P 3000, Morogoro, Tanzania*

*Simu: +255 754501541*

*Email: epinav@suanet.ac.tz*


# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

EPINAV

Enhancing Pro-poor Innovations in Natural Resources and Agricultural Value-chains

# TATHMINI YA MFUMO WA UTOAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO KWA WAKULIMA KUPITIA RUZUKU TANZANIA




AGOSTI 2013

## 1.0 UTANGULIZI

Mojawapo ya kikwazo kikubwa kinacho mkwamisha mkulima mdogo kulima kwa tija ni kumudu gharama za matumizi ya pembejeo za kilimo (mbolea na mbegu bora). Katika kuhakikisha Serikali ya Tanzania inamsaidia mkulima kumudu gharama hizo, mwaka 2008/2009 Serikali ilianzisha na kutekeleza utaratibu wa kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo kwa njia ya ruzuku kwa kupitia mfumo wa vocha (National Agricultural Inputs Voucher System – NAIVS). Katika kufuatilia ufanisi wa mpango huu, utafiti umefanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) chini ya mradi wa **Enhancing Pro-poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chains (EPINAV).**

## 2.0 MADHUMUNI YA UTAFITI

Dhumuni kuu la utafiti ni kutathmini mfumo wa utoaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wadogo kwa utaratibu wa vocha ili kubaini vikwazo, changamoto na hatimaye kupendekeza maboresho mahususi yafuatayo:

- Kutathimini mfumo husika wa usambazaji pembejeo chini ya utaratibu wa vocha
- Kutathimini ufanisi wa mfumo wa usambazaji wa pembejeo kiuchumi
- Kuangalia matokeo ya mfumo huu wa usambazaji wa pembejeo katika maeneo ya uzalishaji wa mazao nafaka ya chakula, uhakika wa chakula na hali ya kipato katika ngazi ya kaya kwa kuzingatia jinsia
- Kutathimini kama utoaji wa pembejeo hizo ulizingatia mahitaji na matakwa halisi ya wakulima
- Kutoa mapendekezo kwa Serikali na wadau mbalimbali namna ya kuboresha mfumo huu kwa wakulima nchini

## 3.0 NINI KILICHOFANYIKA KATIKA UTAFITI HUU?

- Kuandaa zoezi zima na kujipanga kuendesha utafiti huu.
- Ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, maafisa ugani, mawakala wa pembejeo, watawala kutoka halmashauri na idara za kilimo kutoka mikoa ya Shinyanga, Mbeya na Rukwa na pia kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula.
- Warsha za wadau mbalimbali wanaohusika na usambazaji wa pembejeo za kilimo.
- Uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa ili kupata nini kimetokea.

## 4.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Mfumo wa Usambazaji

- Utafiti unaonyesha kuwa mfumo wa usambazaji wa vocha ambao unahusisha ngazi ya Wizara hadi Vijiji umekuwa na urasimu mkubwa mno. Urasimu huu umesababisha pembejeo hizo kuchelewa kuwafikia walengwa na hivyo kutoa mwanya kwa ubadhirifu ambao huchukua sura mbalimbali.
- Uteuzi wa mawakala wa kusambaza pemebjeo pia hauko wazi na unashindwa kubaini wale wasio waaminifu.
- Wakulima wadogo wadogo hawajaelewa bayana namna mfumo huu wa vocha unavyofanya kazi. Hawakupewa elimu juu ya uendeshaji wa mfumo wa vocha za pemebejeo za kilimo.
- Wakulima wadogo hawana uwezo kununua pembejeo hizi na hivyo kuuziwa wakulima wakubwa ambao sio walengwa wakuu wa mfuko huu.
- Wakulima hulazimika kununua pemebejeo ambazo hawazihitaji kwa kuwa hutakiwa kununua furushi lote la pembejeo yaani mbolea, mbegu na madawa.
- Pembejeo huchelewa kufika kwa wakati kulingana na mwenendo wa msimu. Mfano mbolea huja wakati mimea imeishakua.

### 4.2 Tija katika uzalishaji wa mazao, ongezeko la chakula na kipato cha kaya

- Utafiti unaonyesha kuwa kwa wale wachache waliofikiwa kwa wakati na kutumia pembejeo ipasavyo, uzalishaji wa mazao kwa eneo umeongezeka.
- Hata hivyo matokeo yameangaliwa kwa kuongezeka mavuno bila kuangalia faida na hasara katika kununua na kutumia pembejeo hizi.